# RUSHWA NCHINI

K.M.A. Mbehoma

Wahusika: -Mpiga mbiu (MM)
-Meneja (M)
-Kijana 1. (KI)
-Kijana 2. (K2)
-Polisi (P)
-Hakimu (H)
-Wazee 4 (W)

I

MM: Limelia la mgambo, kuhusu rushwa nchini,
Limelia lina mambo, wazembe wawe mbaroni,
Wazembe wala makombo, ya watu walio duni,
Komesha rushwa nchini, bwanyenye wajaza tumbo.

Rushwa adui wa haki, mla rushwa ni adui,
Rais wetu hataki, mla rushwa ni adui,
mwayarundika malaki, umma hamuutambui,
Mla rushwa ni adui, ni adui wa taifa.

Ni adui wa taifa, asiyejua halali,
Nchi mwaipa kashfa, kwa CHAMA na serikali,
Mnaiharibu sifa, ya karibu na ya mbali,
Mla rushwa ni adui, wa serikali na CHAMA.

M: CCM tule sana, siku zetu zimekwisha,
Za CHAMA kuja tubana, walevi kutusafisha,
Wenyewe twajua sana, wala hawatatutisha,
Siku zetu zimekwisha, ni lazima tule sana.

CCM ngumu sana, mambo yake yanachosha,
Kodi nyingi panapana, tena zinasikitisha,
Kwa nini wanatubana, tushindwe kujitunisha?
Tutachoka na maisha, kwa matatizo mapana.

Jana nililewa sana, pesa zimeishaisha,
Sasa njaa yanibana, ninashindwa kujilisha,
Pa kukopa tena sina, janja yangu imekwisha,
Mbinu nimetayarisha, atokeapo kijana.

KI: Ndugu kwako ninafika, kuhusu ombi la kazi,
Na barua nimeshika, yaeleza wazi wazi,
Nakuomba kuridhika, ili nipatiwe kazi,
Nami nipatiwe kazi, nihudumie shirika.

M: Kama ungetaka kazi, ungeenda Mtukula,
Nafasi ingali wazi, usichelewe muhula,
Uhudumie wazazi, kwa malazi na chakula,
Ebu nenda Mtukula, nafasi ingali wazi.

KI: Mtukula nako mbali, mpakani mwa Uganda,
Katika kujali hali, wala si katika kwenda,
Hasa ni katika mali, sina pesa za kuranda,
Sielewi la kutenda, nijulishe tafadhali.

M: Huzijui CCM, zile noti za kisasa?
Nami nipate sehemu, yangu inayonipasa
Iwe kwangu chemchemu, mifuko nikapapasa,
Nikupe kazi ya mana, ebu toa CCM.

KI: Hewala bwana meneja, yote nimeyasikia,
Ntajaribu kidhi haja, wapo Halima jalia,
Siku kwa kutoitaja, nitawahi kadiria,
Nitazidi omba dua, nikidhiwe matilaja.

II

KI: Umma unalalamika, viongozi wahakiki,
Nami nimehamanika, japo natetea haki,
Dunia imechafuka, bila rushwa haushiki,
Nataka hakiki haki, japo unga nautaka.

K2: Vipi ndugu yangu Choma, lipi linalokutasa?
Kumetokea dhuluma, au wamekunyanyasa?
Au nani kakutuma, ukatokea mkasa?
Toa shida yako hasa, iliyokupa husuma.

K1: Ndugu yangu sikiliza, upate kuniauni,
Nimefika kwenye meza, kwa meneja ofisini,
CCM kahimiza, haraka niwe kazini,
Nipe mbinu za kuwini, zipate kunituliza.

CCM hiyo noti, wala si kadi ya CHAMA,
Ajaze katika koti, mradi afanye njama,
Sasa nipige ripoti, Polisi na mahakama?
Haja yangu usalama, kwa taifa siyo noti.

K2; Kweli ingilia kati, kuokoa maamuma,
Tena fanya harakati, zitoke hizi dhuluma,
Kwa moyo ulio dhati, tukwepe zao hujuma,
Wachache wanyonya umma, mbinu zao ni tamati.

III

K1: Tazama bwana Polisi, nataka kudhulumiwa,
Kule kufika ofisi, ya meneja Majaliwa,
Kumetokea nafasi, ya kazi ninatakiwa,
CCM nadaiwa, ya noti nilivyohisi.

P: Yote hayo nilihisi, yatakuja simuliwa,
Ilivyo hali halisi, serikali yaelewa,
Ilingoja mdadisi, amebaki kuendewa,
Pesa namba zitapewa, tumtie kwenye fosi.

K1: Tena bila wasi wasi, nafasi nitapatiwa,
Kadai iwe upesi, haraka kwa kuwahiwa,
Unasemaje Polisi, nisizidi kuchelewa?
Pesa namba zingepewa, tumtie kwenye fosi.

P: Pokea pesa kijana, mpe katika ofisi,
Kisha angalia sana, nje tutabana sisi,
Epuka kukulikana, tupe ishara kihisi,
Tufanye hima upesi, bwenyenye twataka bana.

IV

K1: Bwana ninakuja tena, kusudi tuelewane,
Nafuata ulonena, nilopata tugeane,
Hali yangu duni sana, bwana tusameheane,
Bwana tuajiriane, kwa kiasi hicho bwana.

Ebu shika taslimu, ebu shika hizi pesa,
Kisha ufanye muhimu uniajiri kabisa,
Niwe mpokea simu, kwenye ofisi ofisa,
Unipe kazi ya mana, kwa hizi CCM.

M: Wewe mpokea simu, hiyo ni yako ofisi,
Akili zako timamu, si muhuni nakuhisi,
Kijana tunza nidhamu, tunza siri za ofisi,
Na usiwe mdadisi, mambo yangu kwa kaumu.

K1: Askari nimefika, yote nimeyatimiza,
Kibunda nimezibuka, zamu yako tekeleza,
Kichelewa ataruka, halafu hutamuweza,
Hima nenda tekeleza, apatikane haraka.

P: Meneja ninakushika, upo chini ya Polisi,
Kwa rushwa unahusika, upelekwe mahabusi,
Huoni haya hakika, kuufanya ufilisi!
Nitachunguza jangiri, noti zote zitashika.

Tabia zako ni mbaya, kwa dhuluma umezidi,
Isitoshe huna haya, kueneza uhasidi,
Sasa hapa unagwaya, mithili mwenye baridi,
Umma unajitahidi, kuondoa ukayaya.

Kibwanyenye mhusika, leo utatutambua,
Kwa rushwa umesifika, serikali imejua,
Twende unahitakika, hakimu kuhukumia,
Dhuluma umezidia, yatubidi kukushika.

M: Tafadhali askari, mahakama kwangu chungu,
Usije kunipa shari, pokea hiki kifungu,
Pokea hii sukari, nisamehe ndugu yangu,
Nina mke na wanangu, upweke kwao hatari.

P: Angalia baradhuli, wazo lako duni kwangu,
Angalia ewe nduli, mimi sitaki majungu,
Maneno ya kifedhuli, nitakuchapa marungu,
Kwanza nakutia pingu, kwani rushwa si halali.

V

H: Marembeka Majaliwa, mshtakiwa mhusika,
Kwa rushwa washtakiwa, na Jamhuri hakika,
Umma unadhulumiwa, na wewe kwenye shirika,
Shtaka lakatalika, au linakubaliwa?

M: Shtaka lakataliwa, ninakataa hakika,
Mimi bure nachukiwa, na wakubwa wa shirika,
Ni chuku nasingiziwa, kwa kazi ninasifika,
Ninakataa shtaka, Jamhuri kunishika.

H: Mshtakiwa hataki, makosa kayakataa,
Jambo kwako limebaki, Polisi kuliandaa,
Kuelezea kwa haki, mahakama bila waa,
Mahakama tapokaa, itahukumu kwa haki.

P: Ijapokuwa hataki, makosa kayakataa,
Nina shahidi wa haki, mapesa aliyotwaa,
Nambari tulizimaki, kijana tukamwandaa,
Baada ya kusambaa, dhulumaze kwenye haki.

H: Shahidi aitwee!!!
(Shahidi anaapishwa)
Eleza ulivyoona, mambo kwa kinaganaga,
Ukweli watakikana, dhahiri bila kusaga,
Bila ukweli kubana, iwe kinagaubaga,
Eleza kinaganaga, ukweli watakikana.

K1: (Shahidi): Nilienda omba kazi, kwa meneja Majaliwa,
Kisha nilifata ngazi, zote zilizotakiwa,
Nilikuwa kinywa wazi, hongo nilipodaiwa,
Ndipo niliwajibiwa, Polisi kumpa kazi.

Ndipo nilimpa kazi, uchunguzi kufanyiwa,
Tena ilianza juzi, na noti kunakiliwa,
Meneja si mgunduzi, kwake zikapokelewa,
Polisi hakuchelewa, kambeba wazi wazi.

H: Wazee mwakaribishwa, uwanjani kuingia,
Maoni yakaribishwa, yote mmeyasikia,
Uamuzi wapitishwa, katika hii hatia,
Maoni kwenye hatia, hukumu ije pitishwa.

W: Hakimu unajulishwa, kuhusu hii kadhia,
Hukumu ingepitishwa, Majaliwa yu hatia,
Na fundisho kufundishwa, ili asije rudia,
Hakimu twaamulia, mkosa angefundishwa.

H: Na wewe mshtakiwa,
Nafasi unaipewa,
Utetezi watakiwa,
Adhabu usije pewa.

M: Nakueleza hakimu,
Ninaye mwali nyumbani,
Mimi mshika hatamu,
Ili nikamtunzeni.

H: Kulingana ushahidi, kakosa mshtakiwa,
Ni kosa baya zaidi, rushwa ikipokelewa,
Majaliwa inabidi, adhabu kali kupewa,
Miaka tano wapewa, na kazi ngumu zaidi.

(Ngonjera hii ilipata ushindi wa kwanza katika mashindano ya makombania ya mwaka 1978; huko Bulombora 19KJ; chini ya uongozi wa Ndugu I. Aimo)